# SHERIA YA MABADILIKO YA NANE KATIKA KATIBA YA ZANZIBAR

## YALIYOMO


| KIFUNGU | MAELEZO |
| --- | --- |
| 1. | Jina Fupi na Kuanza Kutumika. |
| 2. | Mabadiliko ya Katiba. |
| 3. | Mabadiliko ya Kifungu cha 5. |
| 4. | Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 5A. |
| 5. | Mabadiliko ya Kifungu cha 6. |
| 6. | Mabadiliko ya Kifungu cha 7. |
| 7. | Mabadiliko ya Kifungu cha 10. |
| 8. | Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 10A. |
| 9. | Mabadiliko ya Kifungu cha 12. |
| 10. | Mabadiliko ya Kifungu cha 13. |
| 11. | Mabadiliko ya Kifungu cha 19. |
| 12. | Mabadiliko ya Kifungu cha 20. |
| 13. | Mabadiliko ya Kifungu cha 22. |
| 14. | Mabadiliko ya Kifungu cha 24. |
| 15. | Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 25A. |
| 16. | Mabadiliko ya Kifungu cha 56. |
| 17. | Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 56A. |
| 18. | Mabadiliko ya Kifungu cha 57. |

19. Mabadiliko ya Kifungu cha 66.

20. Mabadiliko ya Kifungu cha 67.

21. Mabadiliko ya Kifungu cha 68.

22. Mabadiliko ya Kifungu cha 69.

23. Mabadiliko ya Kifungu cha 71.

24. Mabadiliko ya Kifungu cha 89.

25. Mabadiliko ya Kifungu cha 90.

26. Mabadiliko ya Kifungu cha 92.

27. Mabadiliko ya Kifungu cha 94.

28. Mabadiliko ya Kifungu cha 95.

29. Mabadiliko ya Kifungu cha 98.

30. Mabadiliko ya Kifungu cha 99.

31. Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 99A.

32. Mabadiliko ya Kifungu cha 100.

33. Mabadiliko ya Kifungu cha 102.

34. Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 102A.

35. Mabadiliko ya Kifungu cha 103.

36. Mabadiliko ya Kifungu cha 111.

37. Mabadiliko ya Kifungu cha 119.

38. Mabadiliko ya Kifungu cha 134.

39. Mabadiliko ya Kuongeza Kifungu Kipya cha 134A.

40. Mabadiliko ya kuongeza Kifungu Kipya cha Masharti ya Mpito.

**SHERIA NAM. 2 YA 2002**

**NAKUBALI,**

**{ AMANI ABEID KARUME }**
**RAIS WA ZANZIBAR**
**NA**
**MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI**

7th MAY, 2002

# SHERIA YA MABADILIKO YA NANE KATIKA KATIBA YA ZANZIBAR

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

Jina fupi na kuanza kutumika.

1.(1) Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya NANE katika Katiba ya Zanzibar, ya mwaka 2002.

(2) Sheria itaanza kutumika tarehe 1 Mei, 2002.

Mabadiliko ya Katiba.

2. Masharti ya Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 (ambapo katika vifungu vifuatavyo vya Sheria hii itatajwa tu kwa kifupi kama "Katiba") yanabadilishwa kwa namna ilivyoelezwa katika vifungu vya Sheria hii vifuatavyo:-

Mabadiliko ya kifungu cha 5.

3. Kifungu cha 5 kinafanyiwa mabadiliko baada ya neno "kuheshimu" na kuingiza maneno "utawala wa".

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 5A.

4. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 5A baada ya kifungu cha 5:-

"Mgawanyo wa madaraka.

5A(1) Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu, Mamlaka ya Utendaji, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki.

(2) Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya kutekeleza Utoaji Haki ni Mahkama.

(3) Hakuna mamlaka itakayoingilia Mamlaka nyingine isipokuwa kama na kwa kadri ilivyoelezwa katika Katiba hii."

Mabadiliko ya kifungu cha 6.

5. Kifungu cha 6 cha Katiba kinafutwa na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:-

"Mzanzibari.

6.(1) Kutakuwa na Mzanzibari ambaye upatikanaji wake, upoteaji wake na urudishwaji wake atakuwa kama alivyoainishwa katika Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(2) Kila Mzanzibari, kwa misingi ya Katiba hii, ataweza kufaidi haki na fursa zote anazostahiki Mzanzibari, na atapaswa kutekeleza wajibu, majukumu na dhamana za Mzanzibari kama ilivyo kwenye Katiba hii au kwenye Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Mabadiliko ya kifungu cha 7.

6. Kifungu cha 7 cha Katiba kinafutwa na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:-

"Haki ya kupiga kura.

7.(1) Kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar na wananchi. Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya kijifungu cha (2), cha kifungu hichi

pamoja na masharti mengi ya Katiba hii na ya Sheria inayotumika Zanzibar kuhusu mambo ya uchaguzi.

(2) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga Sheria na kuweka masharti yanayoweza kuzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura Kutokana na yo-yote kati ya sababu zifuatazo, yaani Mzanzibari huyo -

(a) kuwa na uraia wa nchi nyingine;

(b) kuwa na ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Mahkama Kuu;

(c) kutiwa hatiani na kuendelea kutumikia adhabu kwa kosa la jinai katika Chuo cha Mafunzo, isipokuwa kwamba mtu aliyewekwa rumande atakuwa na haki ya kuandikishwa kupiga kura;

(d) kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishwaji kama mpiga kura.

(3) Baraza la Wawakilishi litatunga Sheria ya Uchaguzi inayohusu uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani wa Serikali za Mitaa na kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) kuanzisha daftari la kudumu la wapiga kura na kuweka utaratibu wa kurekebisha yaliyomo katika daftari hilo;

(b) kutaja sehemu, nyakati za kuandikisha wapiga kura na muda wa ukaazi katika Jimbo la Uchaguzi kwa ajili ya kupiga kura;

(c) utaratibu wa kumwezesha mpiga kura aliyejiandikisha sehemu moja kupiga kura sehemu nyingine na kutaja masharti ya utekelezaji wa utaratibu huo;

(d) kutaja kazi na shughuli za Tume ya Uchaguzi na utaratibu wa kila uchaguzi ambao utaendeshwa chini ya uongozi na usimamizi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar."

(4) Mbali na sababu zilizoelezwa katika kifungu hiki hakuna sababu nyingine yo-yote inayoweza kumzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura.

Mabadiliko ya kifungu cha 10.

7. Kifungu cha 10 kinafanyiwa mabadiliko yafuatayo:-

(a) kwa kuweka maneno "na maendeleo ya watu na ustawi wa jamii" kati ya neno "umoja" na "katika";

(b) kwa kuongeza mwishoni mwa kijifungu cha (2) maneno "dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka";

(c) kwa kuweka maneno "ana fursa ya kufanya" badala ya neno "anafanya" katika kijifungu cha (7);

(d) kwa kuongeza vijifungu viwili vifuatavyo:-

"(8) Vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa faida na manufaa ya umma na wale wote walio na madaraka watawajibika ama moja kwa moja kwa umma au kupitia kwa vyombo vya uwakilishi.

(9) Vyombo vyote vya Serikali na watumishi wake vitaongozwa na vitazingatia Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu na misingi ya utawala ulio bora."

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 10A.

8. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 10A:-

Matumizi ya masharti ya sura ya pili.

10A. Masharti ya Sehemu hii ya Sura hii hayatatiliwa nguvu ya kisheria na mahkama yo-yote, na mahkama yo-yote nchini haitakuwa na uwezo wa kuamua juu ya suala kama kutenda au kukosa kutenda jambo kwa mtu au mamlaka yo-yote, au kama sheria au hukumu yo-yote, inaambatana na masharti ya Sehemu hii ya Sura hii."

Mabadiliko ya kifungu cha 12.

9. Kifungu cha 12 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko:

(a) Katika kijifungu cha (5) yanawekwa maneno "jinsia"; na kuongezwa mwishoni mwa kijifungu hicho maneno yafuatayo: "isipokuwa kwamba neno "kubagua" halitafafanuliwa kwa namna ambayo itaizuia Serikali kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika jamii".

(b) Kwa kuongeza katika kijifungu cha (6) aya zifuatazo:

"(e) kesi za jinai zinasikilizwa na hukumu kusomwa haraka;

(f) mtuhumiwa katika kesi za jinai anapata fursa ya utetezi wa Wakili aliyemchagua yeye mwenyewe".

Mabadiliko ya Kifungu cha 13.

10. Kifungu cha 13 kinafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kijifungu cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha".

Mabadiliko ya Kifungu cha 19.

11. Kifungu cha 19 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kufuta maneno "za Jamhuri ya Muungano" katika kijifungu cha (2).

Mabadiliko ya Kifungu cha 20.

12. Kifungu cha 20 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza maneno "vyama vya haki za binaadamu" kati ya neno "wafanyakazi" na neno "au".

Mabadiliko ya kifungu cha 22.

13. Kifungu cha 22 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kufuta kijifungu cha (2) na badala yake kuweka:

"(2) Bila ya kujali masharti ya kijifungu cha (1) hakutakuwepo na kazi ya shurti katika Zanzibar".

Mabadiliko ya kifungu cha 24.

14. Kifungu cha 24 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko –

(i) kwa kufuta kifungu cha (1) na badala yake kuweka kijifungu kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(i) Haki na Uhuru wa binaadamu ambayo misingi yake imeorodheshwa na Katiba hii haitatumiwa na mtu mmoja kwa namna ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma na inaweza kubanwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi iwapo tu kibano hicho ni lazima na kunakubalika katika mfumo wa kidemokrasia. Kwa vyo-vyote vile kibano hicho –

(a) hakitaingilia haki ya kutokuteswa, kutoadhibiwa kinyama na kutokudhalilishwa; au

(b) hakitaingilia misingi ya haki yenyewe; au

(c) hakitaileteа jamii athari zaidi ya iliyopo kutokana na jambo ambalo kibano hicho kinalenga."

(ii) kwa kufuta kujifungu cha (2);

(iii) kwa kuongeza maneno "Mahkama Kuu itakuwa na uwezo wa kutoa tamko na kuamuru nafuu au fidia kwa mtu yeyote anayehusika" baadala ya kituo mwishoni kijifungu cha (3);

(iv) kwa kukifanya kijifungu cha (3) kilichopo sasa kuwa kijifungu cha (2);

(v) kwa kuongeza kijifungu kipya cha (3) mara baada ya kijifungu kipya cha (2) kama ifuatavyo –

"(3) Maombi dhidi ya uamuzi wa Mahkama Kuu katika shauri lililofunguliwa dhidi ya masharti ya Sura hii ya Katiba yatasikilizwa na Mahkama Kuu mbele ya Majaji watatu bila ya kumjumuisha Jaji aliyeamua shauri hilo mara ya kwanza. Majaji hao watatu watateuliwa na Jaji Mkuu."

(vi) kwa kufuta kijifungu cha (5).

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 25A.

15. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 25A:-

"Kufungua mashauri.

25A.(1) Mtu yeyote anaweza kufungua shauri katika Mahkama Kuu iwapo ataona kuwa Katiba hii imevunjwa au inavunjwa au inaelekea kuvunjwa. Mahkama Kuu itakuwa na uwezo wa:-

(a) kumtaka Afisa yeyote au chombo chochote cha Serikali kutoa taarifa inayohitajika na Mahkama Kuu yaweza kufanya hivyo kwa kuombwa au kwa uamuzi wake yenyewe;

(b) kutamka na kutoa amri kuwa Katiba hii imevunjwa, inavunjwa au inaelekea kuvunjwa, na Mahkama Kuu inaweza kutoa maagizo kwa Afisa anayehusika au chombo cha Serikali kinachohusika".

Mabadiliko ya kifungu cha 56.

16. Kifungu cha 56 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kama ifuatavyo:-

(a) vijifungu (2) hadi (7) vyote vinafutwa;

(b) kijifungu (1) kitasomeka 56.

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 56A.

17. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 56A:-

"Mkurugenzi wa Mashtaka.

56A(1)(a) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Mashitaka ambaye atateuliwa na Rais.

(b) Mkurugenzi wa Mashtaka atashika wadhifa wake kwa kipindi cha miaka mitano na ataweza kuteuliwa tena kwa vipindi vyengine vya miaka mitano mitano.

(2) Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Mashitaka mpaka awe na sifa za kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahkama Kuu.

(3) Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa na uwezo wa kufanya haya yafuatayo –

(a) kufungua na kushughulikia mashtaka yoyote ya jinai dhidi ya mtu yeyote mbele ya Mahkama yoyote (isipokuwa ya Kijeshi) kuhusiana na kosa lolote ambalo mtu huyo anashtakiwa nalo.

(b) kuchukua na kuendeleza mashtaka yoyote ya jinai ambayo mwanzoni yalifunguliwa na mtu au chombo chengine; na

(c) kusitisha mashtaka yoyote ya jinai ambayo yalianzishwa na mtu yeyote au chombo chochote.

(4) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kijifungu (3) yanaweza kutekelezwa na Mkurugenzi wa Mashtaka mwenyewe au na watu wengine kwa maagizo au amri maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

(5) Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya aya (b) na (c) ya kijifungu (3) yatakuwa mikononi mwake na hayataingiliwa na mtu yeyote au chombo chochote. Isipokuwa pale ambapo mtu mwingine au chombo chengine kimefungua mashtaka ya jinai, basi hakuna chochote katika kijifungu hiki kitakachozuia kufutwa kwa mashtaka hayo na mtu au chombo kilichoshtaki kwa idhini ya Mahkama.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, rufani yoyote kutokana na hukumu katika kesi ya jinai yoyote kwenye Mahkama yoyote, au suala lolote la kisheria lililoachiwa kwa ajili ya mashtaka hayo kufikishwa kwenye Mahkama nyingine, itahesabiwa kuwa ni sehemu ya mashtaka hayo. Kwa kuzingatia kwamba yale mamlaka ya

Mkurugenzi wa Mashtaka chini ya kijifungu (3)(c) hayatatekelezwa kwa ajili ya rufani yoyote ya mtu ambaye amehukumiwa katika kosa la jinai lolote kuhusiana na suala lolote la kisheria lililowekwa makusudi kwa ajili ya mtu huyo.

(7) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwingine yeyote au Idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo haya ya kifungu hiki hayatazuia Mahkama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mkurugenzi wa Mashtaka ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au siyo.

(8) Katika kutumia uwezo wake chini ya kifungu hiki, Mkurugenzi wa Mashtaka atatilia maanani umuhimu wa maslahi ya Taifa kwa kutaka kuona haki inatekelezwa na nia yake ya kuzuia utumiaji mbaya wa vyombo vya kisheria inatimizwa.

(9) Mkurugenzi wa Mashtaka hatoweza kuondolewa ndani ya kipindi chake cha miaka mitano isipokuwa kwa sababu na utaratibu uliowekwa kuondolewa Jaji wa Mahkama Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 95 cha Katiba hii.

(10) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) Mwenendo wa mashtaka kwa ujumla;

(b) Afisa au mtu mwingine yo-yote mwenye sifa ambae Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kukasimu madaraka yake;

(c) utaratibu wa kukata rufaa na muda wa kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahkama yoyote katika kesi ya jinai;

(d) utaratibu wa kuanzisha au kufungua shtaka na mtu binafsi au na taasisi za Serikali na zisizokuwa za Serikali;

(e) kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuingilia au kujaribu kuingilia utekelezaji wa madaraka ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa Katiba hii au Sheria yoyote."

Mabadilio ya kifungu cha 57.

18. Kifungu cha 57 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kw kuweka maneno "na Mkurugenzi wa Mashtaka" kati ya neno "Mkuu" na "hatoanza".

Mabadiliko ya kifungu cha 66.

19. Kifungu cha 66 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza maneno yafuatayo:

"Isipokuwa kwamba Wajumbe wasiopungua wawili watateuliwa na Rais kwa kushauriana na Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi."

Mabadiliko ya kifungu cha 67.

20. Kifungu cha 67 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kukifuta chote na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"67.(1) Kutakuwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanawake kwa idadi ya asilimia thelethini (30%) ya wajumbe wote wa kuchaguliwa katika majimbo ya uchaguzi ambao ni Wazanzibari na ambao watapendekezwa na vyama vya siasa vinavyowakilishwa katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki.

(2) Kila chama cha siasa kitakachoshinda zaidi ya asilimia kumi (10%) ya viti vya majimbo katika Baraza la Wawakilishi kitapendekeza idadi ya majina ya wanachama wanawake kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa uwakilishi baina ya vyama vilivyoshinda uchaguzi katika majimbo na kupata viti katika Baraza la Wawakilishi na kupeleka majina na sifa zao kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

(3) Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, baada ya kuridhika kuwa mwanamke aliyependekezwa ana sifa za kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 68 cha Katiba hii, itamtangaza mara moja mwanamke huyo kuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Isipokuwa kwamba ieleweke kuwa katika kufanya hesabu ya idadi ya Wajumbe wa kila chama cha siasa kila sehemu iliyozidi nusu ya Mjumbe itachukuliwa kuwa ni mjumbe kamili."

Mabadiliko ya kifungu cha 68.

21. Kifungu cha 68 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kufuta maneno "ama Bunge la Jamhuri ya Muungano" katika kijifungu (e).

Mabadiliko ya kifungu cha 69.

22. Kijifungu cha 69 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko:-

(i) Kijifungu cha (1) kinafutwa na badala yake kuweka kifungu kufuatacho:-

"(1) Hakuna mtu atakayechaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa mtu huyo;

(a) ana uraia wa nchi nyingine; au

(b) Mahkama Kuu imeamua, baada ya kushauriwa na Daktari Bingwa wa magonjwa ya akili, kuwa ana ugonjwa wa akili; au

(c) si mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama; au

(d) ametiwa hatiani na kupelekwa Chuo cha Mafunzo au Gereza la Tanzania Bara kwa kosa la jinai kwa kipindi cha kuanzia miezi 6 na zaidi au kosa la uchaguzi linalohusu uaminifu ndani ya miaka mitano kabla ya uchaguzi."

(ii) Vijifungu vya (3), (4) na (6) vya kifungu cha 69 vinafutwa;

(iii) Kwa kukifanya kijifungu cha (5) kilichopo sasa kuwa kijifungu cha (3) na kijifungu cha (7) kuwa kijifungu cha (4).

Mabadiliko ya kifungu cha 71.

23. Kifungu cha 71 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kama ifuatavyo:-

(a) katika kijifungu (1) kwa kufuta aya ya (c) na kuweka aya ya (c) mpya ifuatayo:-

"(c) ikiwa Mjumbe Mwakilishi atakosa kuhudhuria Mikutano ya Baraza mitatu mfululizo bila ya ruhusa ya spika."

(b) katika kijifungu (1) kwa kubadilisha (i) na kusomeka kuwa (e), (ii) kusomeka kuwa (f) na (e) kusomeka kuwa (g);

(c) kuongeza kijifungu kipya cha (2) mara baada ya kijifungu cha (1) kama ifuatavyo:-

"(2) Spika wa Baraza la Wawakilishi atatoa taarifa rasmi kwa Baraza na kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kuhusu kiti cha Mjumbe Mwakilishi kuwa wazi katika kutekeleza masharti ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki."

(d) kwa kukifanya kijifungu cha (2) kilichopo sasa kusomeka kuwa ni kijifungu cha (3).

Mabadiliko ya kifungu cha 89.

24. Kifungu cha 89 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kukiondoa kifungu hichi na kuweka kipya kifuatacho:-

"Kuitisha Mkutano wa Baraza.

89(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hichi, mkutano wa Baraza utakuwa sehemu yoyote katika Zanzibar na utafanyika wakati wowote ambapo Rais ataamuru.

(2) Kutakuwa na mkutano wa Baraza la Wawakilishi angalau mara moja kila mwaka na kipindi cha miezi kumi na mbili hakitopita baina ya mkutano mmoja na mwingine."

Mabadiliko ya kifungu cha 90.

25. Kifungu cha 90 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kuondoa kijifungu (1) na kuweka kipya kifuatacho:-

"(1) Wakati Baraza litakapovunjwa, Uchaguzi Mkuu wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi utafanywa na mkutano wa mwanzo wa Baraza jipya utafanywa si zaidi ya siku tisini toka kuvunjwa kwa Baraza."

Mabadiliko ya kifungu cha 92.

26. Kifungu cha 92 cha Katiba kinafanyiwa Mabadiliko kwa kuongeza kijifungu cha (3) kipya kama ifuatavyo:-

"(3) Kukitokea hali ya hatari au kama kuna hali ya hatari ambayo Rais anaona inasababisha kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi na iwapo wakati huo Baraza la Wawakilishi limevunjwa na matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu hayajatangazwa basi Rais aweza kutoa Taarifa Maalum ya kuitisha Mkutano wa Baraza la Wawakilishi na kuagiza kwamba Spika na watu wote waliokuwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mara tu kabla ya Baraza la

Wawakilishi halijavunjwa wahudhurie Mkutano huo na watahesabiwa hivyo mpaka usiku wa manane wa siku yatakapotangazwa matokeo ya kura zilizo nyingi za Uchaguzi Mkuu."

Mabadiliko ya kifungu cha 94.

27. Kifungu cha 94 cha Katiba kinafanyiwa Mabadiliko yafuatayo:-

(a) kwa kuongeza mara baada ya kijifungu cha (5) kijifungu cha (6) kifuatacho:-

"(6)(a) Rais anaweza kumteua mtu yeyote kuwa Kaimu Jaji wa Mahkama Kuu kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au Jaji wa Mahakama Kuu kwa mkataba wa kipindi maalum kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi ya Mahkama.

(b) Masharti ya Kazi, marupurupu na kiinua mgongo cha Jaji kwa mkataba wa kipindi maalum yataamuliwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama."

(b) kwa kuongeza maneno "kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu na baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama" mwishoni mwa kijifungu cha (1);

(c) kwa kufuta maneno "baada ya kushauriana na" na badala yake kuweka maneno "kutokana na mapendekezo ya" katika kijifungu cha (2);

(d) kwa kuongeza maneno "au Kaimu Jaji" kati ya neno "jaji" na "wa" katika kijifungu cha (3);

(e) kwa kuongeza kijifungu cha (7):-

"(7) Jaji Mkuu hatoweza kuondolewa kwenye kiti cha Jaji Mkuu isipokuwa kwa sababu na utaratibu uliowekwa kuondolewa Jaji wa Mahkama Kuu kwa mujibu wa kifungu cha 95 cha Katiba hii."

Mabadiliko ya kifungu cha 95.

28. Kifungu cha 95 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kama ifuatavyo:-

(a) kwa kufuta kijifungu cha (1) na kuweka badala yake kijifungu kipya cha (1) kifuatacho:-

"(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki Jaji wa Mahkama Kuu ataendelea kushika wadhifa wake hadi kufikia umri wa miaka sitini ambapo anaweza kustaafu kwa hiari ama kuendelea hadi kufikia umri wa miaka sitini na tano ambapo atastaafu kwa lazima."

(b) kwa kuongeza mara baada ya kujifungu kipya cha (1) kijifungu cha (2) kama ifuatavyo:-

"(2) Bila ya kuathiri masharti ya kijifungu cha (1) ya kifungu hiki, Rais kwa kushauriana na Tume ya Utumishi ya Mahkama anaweza kumteua tena Jaji aliyekwisha staafu kushika madaraka ya Jaji wa Mahkama Kuu kwa muda au kwa ajili ya kesi maalum."

(c) kwa kuvifanya vijifungu vya (2), (3), (4), (5) na (6) kuwa vijifungu vya (3), (4), (5), (6) na (7).

(d) kwa kuongeza kijifungu cha (8) kama ifuatavyo:-

"(8) Jaji Mkuu au Jaji wa Mahkama Kuu hatateuliwa au kuchaguliwa kufanya kazi nyengine katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au sehemu nyingine yoyote kwa kipindi cho-chote kile bila ya ridhaa yake kwa maandishi."

Kufuta kifungu cha 98.

29. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kufuta kifungu cha 98.

Mabadiliko ya kifungu cha 99.

30. Kifungu cha 99 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kukifuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:-

"Kazi na uwezo wa Mahkama ya Rufaani.

99 Mahkama ya Rufaani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na uwezo wa kusikiliza rufaani toka Mahkama Kuu ya Zanzibar isipokuwa kesi zozote zinazohusika na:-

(a) tafsiri ya Katiba hii;

(b) mambo ya Kiislamu ambayo yameanzia katika Mahkama za Kadhi;

(c) mambo mengine yoyote yaliyoainishwa katika Katiba hii na sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 99A.

31 Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 99A kifuatacho:-

"Ufafanuzi wa Katiba kupelekwa Mahkama Kuu.

99A(1) Iwapo katika shauri lolote katika Mahkama yoyote iliyo chini ya Mahkama Kuu suala la tafsiri ya Katiba hii litajitokeza, suala hilo mara moja litawasilishwa Mahkama Kuu kwa uamuzi na shauri hilo halitaendelea mpaka uamuzi wa Mahkama Kuu uwe umepatikana.

(2) Maombi dhidi ya uamuzi wa Mahkama Kuu juu ya suala la tafsiri ya Katiba hii yatasikilizwa na Mahkama Kuu mbele ya Majaji watatu bila ya kumjumuisha Jaji aliyeamua suala hilo mara ya kwanza. Majaji hao watatu watateuliwa na Jaji Mkuu."

Mabadiliko ya kifungu cha 100.

32. Kifungu cha 100 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kufuta kijifungu cha (2).

Mabadiliko ya kifungu cha 102.

33. Kifungu cha 102 cha Katiba kinafanyiwa Mabadiliko:-

(i) Kwa kufuta kijifungu cha (1) na badala yake kuweka kufuatacho:-

"(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Jaji Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Jaji mmoja wa Mahkama Kuu aliyeteuliwa na Rais;

(c) Jaji mmoja mstaafu wa Mahkama Kuu au Mahkama ya Rufaani ya Tanzania aliyeteuliwa na Rais;

(d) Wakili mmoja aliyeteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya Chama cha Wanasheria Zanzibar;

(e) Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi Serikalini;

(f) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(g) Kadhi Mkuu; na

(h) Mtu mwengine yeyote ambaye Rais ataona anafaa."

(ii) Kwa kuongeza vijifungu vipya vya (2) na (3) mara baada ya kijifungu kipya cha (1) kama ifuatavyo:-

"(2) Mtu yeyote hatoweza kuteuliwa chini ya kijifungu (c), (d) na (h) cha kifungu hiki iwapo ni mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au amezuiliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

(3) Mjumbe wa Tume ya Utumishi ya Mahkama hatoweza kuondolewa isipokuwa kwa sababu ya tabia mbaya au kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake kutokana na maradhi ya mwili au akili yaliyothibitishwa na Bodi ya Utabibu ya Madakatari wasiopungua watatu."

(iii) Kwa kuvifanya vijifungu vya (2) na (3) kuwa vijifungu vya (4) na (5).

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 102A.

34. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu kipwa cha 102A kifuatacho:-

"Uwezo wa Tume ya Utumishi ya Mahkama.

102A. Tume ya Utumishi ya Mahkama itakuwa na uwezo wa:-

(a) kumshauri Rais juu ya uteuzi wa Jaji Mkuu; na

(b) kupendekeza kwa Rais uteuzi wa Jaji wa Mahkama Kuu."

Mabadiliko ya kifungu cha 103.

35. Kifungu cha 103 kinafanyiwa mabadiliko yafuatayo:-

(a) kwa kuongeza maneno yafuatayo baada ya kijifungu cha (1);

"Isipokuwa Jaji Mkuu hatokuwa Mwenyekiti wa mkutano wowote wa kinidhamu, na wajumbe wa Tume watamchagua Mwenyekiti kutoka miongoni mwao."

(b) kwa kufuta kijifungu cha (2);

(c) kwa kuongeza vijifungu vya (4), (5), na (6):-

"(4) Tume ya Utumishi ya Mahkama itakuwa na uwezo wa kupendekeza mishahara, marupurupu na mafao ya uzeeni ya Majaji na Mahakimu.

(5) Jaji Mkuu atakuwa na uwezo wa kuwahamisha Mahakimu. Hakimu yoyote asiyeridhika atakuwa na uwezo wa kukata rufaa kwenye Tume ya Utumishi ya Mahkama.

(6) Baraza la Wawakilishi laweza kutunga sheria kuhusu mambo yafuatayo:-

(a) utaratibu wa mikutano ya Tume ya Utumishi ya Mahkama; na

(b) marupurupu na mafao mengine ya wajumbe wa Tume; na

(c) mambo mengine yanayohusu Tume ya Utumishi ya Mahkama."

Mabadiliko ya kifungu cha 111.

36. Katiba inafanyiwa mabadiliko katika kifungu cha 111 kwa kuongeza katika kijifungu cha (5):-

(a) neno "Spika" baina ya maneno "Waziri Kiongozi" na "Jaji Mkuu",

(b) maneno "Kadhi Mkuu" baina ya maneno "Majaji wa Mahkama Kuu" na "Majaji wa Rufaa";

(c) maneno "Mkurugenzi wa Mashtaka" baina ya maneno "Mwanasheria Mkuu" na "Mdhibiti".

Mabadiliko ya kifungu cha 119.

37. Kifungu cha 119 cha Katiba kinafanyiwa Mabadiliko yafuatayo:-

(i) Kwa kufuta kijifungu cha (1) na badala yake kuweka kifuatacho:-

"(1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kwa utaratibu atakaoona unafaa;

(b) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa shughuli za Serikali kwenye Baraza la Wawakilishi;

(c) Wajumbe wawili watakaoteuliwa na Rais kufuatana na mapendekezo ya Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi;

(d) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu;

(e) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kama Rais atakavyoona inafaa;

(ii) Kwa kufuta kijivungu (2) na kuweka kifuatacho:-

(2)(a) Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi atakuwa mtu aliyekuwa au mwenye sifa za kuwa Jaji katika Mahkama Kuu au Mahkama ya Rufaa katika nchi yoyote iliyo mwanachama wa Jumuiya ya Madola au mtu anayeheshimika katika jamii;

(b) Tume ya Uchaguzi itamteua Makamo wa Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wajumbe wake."

(iii) Kwa kufuta kijifungu cha (4) na badala yake kuweka:-

"(4) Bila ya kuathiri masharti mengine ya kifungu hiki, mjumbe wa Tume ya Uchaguzi atasita tu kuwa mjumbe litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo:-

(a) ukimalizika muda wa miaka mitano tangu alipoteuliwa; au

(b) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo kama asingekuwa mjumbe lingemfanya asiweze kuteuliwa kuwa mjumbe wa Tume ya Uchaguzi.

(iv) Kwa kufuta kijifungu cha (10) na badala yake kuweka kifuatacho:-

"(10) Kiwango cha mikutano ya Tume ya Uchaguzi ni Mwenyekiti au Makamo Mwenyekiti na wajumbe wanne; na kila uamuzi wa Tume ni lazima uungwe mkono na wajumbe wa Tume walio wengi."

Mabadiliko ya kifungu cha 134.

38. Kifungu cha 134 cha Katiba kinafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza tafsiri ya "Jaji", "Kikao cha Baraza la Wawakilishi" na "Mkutano wa Baraza la Wawakilishi" kama ifuatavyo:-

"Jaji" maana yake ni Jaji wa Mahkama Kuu na linajumuisha Kaimu Jaji.

"Kikao cha Baraza la Wawakilishi" maana yake ni kikao cha siku moja au sehemu ya siku endapo Baraza halikukaa kwa siku nzima kinachoanza kwa kusomwa dua na kumalizika kwa kuakhirishwa hadi siku inayofuata au siku nyingene ya baadae;

"Mkutano wa Baraza la Wawakilishi" maana yake ni mfululizo wa vikao vya Baraza kuanzia kikao cha kwanza hadi kufikia wakati ambao shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya mkutano huo zitakuwa zinamalizika.

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 134A.

39. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 134A:-

"Kufuta Katiba ya 1979.

134A. Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 1979 imefutwa."

Mabadiliko ya kuongeza kifungu kipya cha 135A cha masharti ya mpito.

40. Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 135A cha masharti ya mpito:-

"Masharti ya mpito.

135A. Bila ya kujali masharti yaliyomo katika Sheria hii na kwa ajili ya kuondoa utatanishi:-

(1)(a) Chombo chochote ambacho muundo wake ama utaratibu wa kuundwa kwake kumebadilishwa na sheria hii chombo hicho kitaendelea kufanya kazi hadi muundo wake utapobadilishwa ama kitapoundwa upya kwa kufuata masharti ya sheria hii;

Isipokuwa kwamba hatua za marekebisho zitachukuliwa mapema kadri inavyowezekana;

(b) Sheria yoyote ambayo imeathirika kutokana na Sheria hii itaendelea kuwa na nguvu na kadri itavyohitajika itatafsiriwa kulingana na sheria hii kwa nia ya kuifanya iendelee kutumika hadi hapo itapofanyiwa marekebisho;

(c) Hatua zitazochukuliwa au zilizochukuliwa na chombo chochote chini ya sheria au utaratibu uliokuwepo kabla ya sheria hii zitakuwa halali na zitajaaliwa kuwa zimefanywa kihalali chini ya sheria hii.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 1(2) cha sheria hii –

(a) Masharti ya kifungu cha 16 na masharti yote yanayohusiana na kuanzishwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hayataanza kutumika hadi tarehe 1 Julai, 2002.

(b) Masharti ya kifungu cha 18 hayataanza kutumika hadi baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa mwaka 2005."

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 16 Aprili, 2002.

**{ KHAMIS JUMA CHANDE }**
**KATIBU**
**BARAZA LA WAWAKILISHI**